**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MKOA WA DODOMA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA NNE - 2023.**

**015 ELIMU YA DINI YA KIISLAM**

**MUDA: SAA 3. Agosti, 2023**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu **A**, **B** na **C**; Jibu maswali yote kutoka sehemu **A** na **B** na maswali mawili kutoka sehemu **C**
2. Sehemu **A** ina alama **16%** sehemu **B** ina alama **54%** na **C** ina alama **30%**
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani
5. Andika namba yako ya mtihani kwa kila ukurasa wa kujibu maswali .

**SEHEMU A. (ALAMA 16)**

1. Jibu maswali yote katika sehemu hii kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi

i. Ni ipi maana ya kumuabudu Allah (s.w) katika maisha ya mwanadamu ya kila siku?
   - A. Kuwa mtumwa au mtumishi wa yeyote
   - B. Kutekeleza swala kila siku
   - **C.** Kumtii Allah s.w kwa unyenyekevu / /
   - D. Kutekeleza nguzo za uislamu kwa usahihi
   - E. Kutii na kuiga mwenendo wa mtume s.a.w

ii. Ni mfumo wa maisha uliojengwa na wanadamu misingi yake ni kukanusha uwepo wa mwenyezimungu s.w
   - A. Dini ya ushirikina
   - B. Dini ya utawa / /
   - C. Dini ya ukafiri
   - D. Dini ya uyahudi
   - E. Dini ya ukristo

iii. Allah s.w alimuumba mwanadamu kwa lengo la kufanya ibada,ni lipi kusudio la kufanya ibada katika uislamu?
   - A. Kupata pepo ya Allah s.w
   - B. Kuepushwa na moto wa Allah (s.w)
   - *C. Kupata radhi za Allah (s.w)*
   - ***D.** Kusamehewa madhambi* / /
   - E. Kupata thawabu na pepo

iv. Wahyi wa mwanzo alioshushiwa mtume muhammad (s.a.w) ulikuwa ukimsisitiza mtume s.a.w juu ya:

A. Kumuamini ALLAH S.W pekee
B. Kujielimisha kwa ajili ya Allah (s.w)
C. Kumcha Allah s.w katika maisha / /
D. Kulingania uislamu katika jamii
E. Kumuabudu Allah s.w ipasavyo

v. Zifuatazo sio sifa za muumini isipokuwa:-

A. Mwenye yakini moyoni na kuthibitisha kwa ulimi
B. Mwenye kutenda mema na kuacha maovu
C. Mwenye kusoma sana Quran na kulia / /
D. Mwenye khofu na mashaka katika maisha yake
E. Mwenye kuamini na kufundisha imani yake kinadharia

vi. Yafuatayo ni matendo ya siku ya kuchinja isipokuwa :

A. Kutupa mawe katika mnara mkubwa
B. Kuchinja mnyama yoyote
**C.** Kusa'i **/ /**
D. Kunyoa kichwa
E. Kutufu tawaful ifadha

vii. Ni ipi tofauti iliyopo kati ya sanda ya mtoto na ile ya mwanamke?

A. Sanda ya mtoto haina gharama sana kuliko ile ya mwanamke / /
B. Sanda ya mtoto ni nyepesi kuliko ya mwanamke
C. Sanda ya mtoto ina vipande vitatu na ya mwanamke ina vipande vitano
D. Sanda ya mtoto ni laini sana
E. Sanda ya mtoto haiuzwi ila ya mwanamke inauzwa.

viii. Vipaji alivyotunukiwa mwanadamu vina nafasi gani katika kumjua mwenyezimungu s.w

A. Kumuwezesha mwanadamu kuujua na kuutekeleza uislamu
B. Kumuwezesha mwanadamu kutumia elimu na akili vizuri / /
C. Kumuwezesha mwanadamu kumtumikia mwenyezimungu (s.w)
D. Kumuwezesha mwanadamu kumtambua mwenyezimungu (s.w)
E. Kumuwezesha mwanadamu kujua mema na mabaya

ix. Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika kuhakiki usahihi wa matini ya hadith isipokuwa:

A. Isipingane na Aya za Quran
B. Isipingane na hadithi nyingine

C. Isipingane na uhalisia
D. Isiwe ndefu ya kuchosha / /
E. Isiwe na maneno ya uwongo

x. Ipi kati ya hizi zifuatazo hueleza namna zakat na sadakat zinavyoitakasa jamii ya kiislamu:
A. Kuiendeleza jamii kiuchumi
B. Kuiendeleza jamii haswa
C. Kuendeleza sera za mtume (s.a.w) / /
D. Kutoa mali nyingi
E. Kutoa vilivyo vya halali

2. Oanisha maneno kutoka orodha **A** na maneno kutoka orodha **B** kisha jaza herufi yake katika karatasi ya kujibia.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| i. Haki za Allah (s.w)<br>ii. Haki za nafsi<br>iii. Haki za viumbe na mazingira<br>iv. Haki za binadamu kwa ujumla<br>v. Haki za raia katika dola ya kiislamu<br>vi. Haki za maadui katika vita | A. Kupanda miti na kutunza misitu<br>B. Kumuabudu allah (s.w)<br>C. Kuishi,kulindwa na kuheshimiwa<br>D. Kuwapa mahitaji yao ya lazima<br>E. Uhuru wa kutoa maoni na kushtaki<br>F. Chakula,malazi,elimu<br>G. Kuwaua wote<br>H. Kupelekwa jela |

**SEHEMU B (ALAMA 54)**

**Jibu maswali yote**

3. (a) Ustadh zayd alielezea kisa cha kusisimua cha mtu aliyeenda **Tawaf** huku akisoma dua na kuikariri dua hiyo mara kwa mara ,hata hivyo aliwaeleza waumini mafunzo matatu yatokanayo na Tawaf.Bainisha kwa kutumia hoja tatu.

(b) Kwa kutumia mifano bainisha aina kuu nne za shirk.

(c) Kwa kutumia hoja mbili eleza kwa ufupi udhaifu wa hoja inayosema kuwa Quran ni mashairi aliyoyatunga muhammad (s.a.w).

4. (a) Kwa kutumia hoja tatu toa ushahidi unaoonesha ufufuo katika maisha ya kila siku.

(b) Bainisha sifa tatu za mashahidi wawili ili ndoa ya kiislamu ifungwe

(c) Wewe kama msomi wa elimu ya dini ya kiislamu umewakuta wanakijiji wanabishana kuhusu kugawa mirathi,pamoja na hivyo wanachobishania ni kitu gani wanatakiwa kuzingatia kabla ya kugawa mirathi? Wabainishie kwa hoja tatu.

5. (a) Wabainishie waislamu kwa kutumia hoja sita mafungu yenye kurithiwa

   (b) Ni ipi hekima ya stara kwa mwanamke? Taja kwa hoja tatu

6. (a) Toa hukumu ya makosa yafuatayo kwa mujibu wa uislamu:
   i. Kuritadi
   ii. Ujambazi
   iii. Kashfa

   (b) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yanavyotumika katika benki za kiislamu.

   i. Musharikah
   ii. Muqaradhah
   iii. Ijara -Uara wa Iktina

7. (a) Taja haki tatu anazostahili raia katika dola ya kiislamu

   (b) *'’Mwenyezimungu amemlaani mtoa rushwa,mpokea rushwa na mtu wa kati baina ya mtoaji na mpokeaji rushwa”* (Ahmad).Bainisha kwa kutumia hoja tatu ulichojifunza katika hadith hiyo.

   (c) Bainisha sifa kuu tatu ili mtu awe kiongozi kwa mujibu wa uislamu

8. (a) Bainisha kwa hoja nne sifa maalumu za mitume wa mwenyezimungu (s.w).

   (b) Taja misingi mikuu mitatu ya haki na uadilifu katika uislamu

   (c) Bainisha sifa mbili za mtu aliyetoa shahada ya kweli katika uislamu

**SEHEMU C: ALAMA 30**
**Jibu maswali mawili tu.**

9. Eleza kwa kutumia hoja sita kwanini matajiri walio wengi hawaendi hijja?
10. Kwa kuzingatia mafunzo yanayopatikana kwa waislamu wa zama za leo kutoka kwa maswahaba wa mtume (s.a.w) walijiimarisha kiuchumi na kusimamia mapato ya serikali ya kiislamu ipasavyo,kwa kutumia hoja sita eleza njia walizotumia maswahaba wa mtume s.a.w kukusanya mapato ili kuimarisha uchumi wa serikali ya kiislamu.
11. Eleza kwa kutumia hoja sita unaweza vipi kuthibitisha kuwa Quran ni kitabu cha

Allah (s.w) kutokana na Quran yenyewe.